



OFISI YA TAIFA YA TAKWIMU

SHINDANO LA MWANDISHI BORA WA HABARI ZA TAKWIMU KWA MWAKA 2023

Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) inaendelea na maandalizi ya Siku ya Takwimu Afrika ambayo huadhimishwa kila tarehe **18 Mwezi Novemba** ya kila mwaka. NBS kwa kutambua umuhimu wa Vyombo vya Habari katika kuelimisha jamii kuhusu shughuli mbalimbali za Kitakwimu, imekuwa ikiandaa Shindano la Waandishi Bora wa Habari za Kitakwimu kila mwaka. Shindano hili lina lengo la kuhimiza uandishi zaidi wa shughuli za kitakwimu pamoja na kuhimiza matumizi ya takwimu katika majukumu ya kila siku. Hivyo basi, NBS inawaalika Waandishi wa Habari kuwasilisha kazi zao walizo zifanya kuanzia **Desemba, 2022** hadi **Novemba 5, 2023** ili ziweze kushindanishwa na kupata Waandishi Bora watatu (3) kwa mwaka huu.

Shindano hili ni kwa **Waandishi walioajiriwa au wakujitegemea wanaofanya kazi na Taasisi mbalimbali kwenye vyombo vya Habari na Mitandao ya Kijamii ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**

Makala/Habari zitakazopokelewa kwa ajili ya shindano hili ni zile zilizochapishwa magazetini na kwenye mitandao inayochapisha habari katika kipindi kilichotajwa kati ya **Desemba, 2022** hadi **Novemba 5, 2023**.

VIGEZO NA SIFA ZA MAKALA/HABARI ZITAKAZO SHINDANISHWA

Iwe ni Makala yenye mchanganyiko wa maandishi, habari picha na vielelezo vyovyote ambavyo vitamfanya mtu aeewe dhumuni la ujumbe na achukue hatua kutokana na ushahidi wa takwimu zilizotolewa. Vigezo vingine ni pamoja na:-

1. Makala/Habari husika iwe na uchambuzi wa kina wa mada inayochambuliwa kuhusu takwimu na iwe kwenye lugha rahisi inayoeleweka;

2. Lugha ya picha inatakiwa iwe rahisi wakati wa kuelezea maudhui ya kilichowasilishwa;
3. Inapaswa kujumuisha vyanzo vyta kuaminika vyta habari ili kuongeza thamani/ladha ya habari inayoelezea takwimu hizo;
4. Makala/Habari iwe yenye Ushahidi wa Takwimu ambazo zimeandaliwa na mwandishi kwa kuchambua na kuhoji ripoti rasmi ya takwimu (**Statistical Report**) ili kupata taarifa au ujumbe zaidi uliokusudiwa katika jamii; na
5. Makala/Habari inapaswa itoe takwimu zenye malengo ya kibinadamu/kumgusa mtu au jamii. Inapaswa izingatie ubinadamu na kujibu swali, kwa nini tunajali?

Washiriki wawasilishe kazi zao kabla ya tarehe **10 Novemba 2023**, saa kumi jioni. Kupitia barua pepe ifuatayo: takwimutanzania@gmail.com
Washiriki pia wawasilishe kiambatisho cha fomu ya ushiriki kilicho jazwa taarifa sahihi kama zinavyohitajika.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na **William Matee** kwa simu namba **0716 621 067** au **Emmanuel Ghula** kwa simu namba **0756 934 356/0789 533 977**.

Tangazo hili limetolewa na:

Ofisi ya Taifa ya Takwimu

S. L. P. 2683,

DODOMA.

*MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI
OFISI YA TAIFA YA TAKWIMU
S.L.P 2683
DODOMA*



**FOMU YA USHIRIKI WA SHINDANO LA MWANDISHI BORA WA
TAKWIMU KWA MWAKA 2023**

UTAMBULISHO WA CHOMBO CHA HABARI

Jina la Chombo cha Habari:

Jina la Mhariri wa Habari:

Namba ya Simu ya Mhariri wa Habari:

UTAMBULISHO WA MSHIRIKI

Jina la Ukoo:

Jina la Kati:

Jina la Kwanza:

MAWASILIANO

Namba ya Simu:

Barua pepe:

Mkoa unakofanya kazi zako za uandishi:

MAKALA/HABARI ILIYOWASILISHWA AU ZILIZOWASILISHWA

1.
2.
3.

MUHURI WA CHOMBO CHA HABARI
